


Clean Energy and Conservation in Kuku Group Ranch

Key Messages



- ⇒ Most families still use firewood to cook. Around 8 out of 10 homes in Kuku depend on firewood, and only 3 out of 10 have electricity.
- ⇒ Our firewood use is destroying forests fast. Every dry season, we cut down trees equal to about 6,500 acres, almost a whole forest. Our schools also burn about 28 acres for cooking, which adds to the problem.
- ⇒ Trees are disappearing. In the year 2000, we had good tree cover of about 14%, but by 2022 it had dropped to 11%. At the same time, bare, dry land has grown from 29% to 56% of our area.
- ⇒ Fewer trees affect our land and animals. When we lose trees, we get less rain, our soil is washed away, and animals like elephants and zebras have nowhere to go.
- ⇒ Women and girls are carrying the biggest burden. Every week, they spend more than 12 hours walking long distances to find firewood. It's tiring, risky, and takes time away from school or rest.

Why We Need Change



- * Kuku Group Ranch still depends too much on firewood for energy.
- * If we don't change this, by 2030 our land will become even more bare, we could lose over 32,000 more acres of trees, which is like cutting 1.6 to 3.3 million trees.
- * This will hurt our land, our wildlife, and our way of life.
- * Right now, most families (70%) don't have electricity, and that might not change unless action is taken.
- * Fuel prices like kerosene and diesel might rise, making life even harder.
- * Also, smoke from traditional cooking fires is making our families sick. The smoke fills homes and causes breathing problems, especially for mothers and young children.



The Way Forward – What We Can Do as a Community



- ◇ **Use Clean Energy at Home:** Try solar lanterns, improved cookstoves, or biogas if possible. Even simple changes like making briquettes can reduce the need for firewood.
- ◇ **Join Local Projects:** Support ongoing work by groups like MWCT or local conservancies. Attend trainings on stoves, solar, or planting trees.
- ◇ **Respect Conservation Rules:** Let's agree and follow our own rules like only collecting dry firewood, avoiding charcoal burning, and planting trees every year.
- ◇ **Support Women and Youth:** Women should lead clean cooking decisions. Youth can help plant trees, spread awareness, and learn new skills.

What We Need from Leaders and Partners:

- ◇ **Include Clean Energy in County Plans:** Ensure development budgets include solar power, LPG access, and reforestation for rural areas like ours.
- ◇ **Give Support and Incentives:** Help us adopt new energy by giving subsidies, loans, or group support to make things affordable.
- ◇ **Provide Trainings and Jobs:** Train our youth on solar installation, biogas systems, and local stove-making to create green jobs.
- ◇ **Link Us to Opportunities:** Make sure Kuku benefits from donor projects, fuel programs, or national plans for rural energy.
- ◇ **Help Us Learn from Others:** Take us to see other communities doing this well so we can learn and try the same here.



Together, We Can Power Conservation



We, the people of Kuku, have the power to shape a better future. By working together, we can stop cutting too many trees, use clean energy like solar and biogas, and bring back our forests. Every person matters from a mother using a clean stove, to a young person planting trees.

Let's imagine a brighter Kuku: homes lit with solar lamps, children breathing clean air, green hills full of trees, and women leading clean energy projects. This is possible if we all play our part, families, elders, youth, and leaders.

We are strong and wise as a community. Now is the time to act. Let's say: Our energy will protect our forests, and our forests will protect our future. If we work together, we can make Kuku a great example of clean living and conservation.

"The best time to plant a tree was 20 years ago. The second best time is now." Let's act today for a better tomorrow "

Reforestation Our Land: Our Role in Tree Planting and Conservation

Reforestation is essential to restoring Kuku's land and securing our environment and energy future. The community can lead this effort by:

- ◇ **Raising Seedlings:** Community nurseries can grow indigenous tree saplings. Women and youth groups can collect seeds and raise them using local knowledge.
- ◇ **Planting Smartly:** Trees should be planted at the start of the rainy season especially near rivers, schools, and homesteads.
- ◇ **Protecting Trees:** Young trees must be guarded from livestock and drought using simple guards like thorn fences or wire mesh. Community members can water them and replace dead seedlings each season.
- ◇ **Involving Everyone:** Tree planting should involve all, especially children and youth.

Clean Energy Options for Kuku:

The Kuku community has great potential for clean energy because of its strong sunlight, many livestock, and hardworking people. Using clean energy can help us meet daily needs while protecting our forests.

◇ Solar Power:

Kuku receives sunlight all year round. Solar energy can be used for lighting, charging phones, running radios, and pumping water. Over half of households already use small solar systems or lanterns. Some villages even use solar to pump water and reduce conflict with wildlife.

◇ Biogas Energy:

Our cows, goats, and sheep produce manure, which can be turned into clean cooking gas using biogas systems. Biogas burns without smoke and gives strong heat. The leftover slurry is a good fertilizer. If more households adopt biogas, we can reduce firewood use and protect our trees.

◇ Briquettes and Improved Cookstoves:

These are better ways of cooking that use less firewood or charcoal. Improved stoves burn more efficiently and make less smoke. They can save up to half the amount of firewood usually used.

Why Clean Cooking is Good for Us

Switching to clean cooking is not just about saving trees as it helps our health, our time, and our land.



◇ We Save Trees

Clean stoves and fuels like briquettes, biogas, or solar cookers use much less wood. If many homes use these, we'll cut fewer trees. Forests will grow back. Our land will stay green, and bare areas can recover.

◇ We Protect Our Health

Open fire smoke in the kitchen causes chest problems, coughing, and stinging eyes. Clean cooking like biogas or improved cookstoves makes less or no smoke. This means healthier homes and better breathing for our families.

◇ We Save Time

Women and girls spend many hours every week looking for firewood. Clean energy means less time walking far or carrying heavy wood. That time can now be used for school, farming, or resting.

Our Energy, Our Forests, Our Future

The choices we make today:

- 1) how we cook,
- 2) what fuels we use,
- 3) how we treat our land,

will shape the future of our families, forests,
and livelihoods.

Let's choose clean energy, protect our environ-
ment, and work together for a healthier, green-
er, and more prosperous Kuku.

The future is in our hands.



KUKU GROUP RANCH


Community Brief: Clean Energy and Conservation in Kuku Group Ranch

Clean Energy and Conservation in Kuku Group Ranch

Lighting our homes,
protecting our trees,
securing our future.



Lighting our homes, protecting our trees, securing our future



KUKU GROUP RANCH

Community Brief
Prepared By: S. Vintage W. Mwangi-
LDE Thesis Lab, University of Nairobi
With support from Nuvoni Centre for
Innovation Research, MWCT and the
Kuku Group Ranch Community.
Email: vintagemwangi5@gmail.com



Clean Energy Options for Kuku



Solar Power



Biogas Energy



Briquettes
and Improved
Cookstove


CLEAN ENERGY AND CONSERVATION IN KUKU GROUP RANCH

Lighting our homes, protecting our trees,
securing our future.



Nishati Safi na Uhifadhi wa Mazingira katika Ranchi ya Kuku

Ujumbe Muhimu kwa Jamii Yetu



- ⇒ Familia nyingi bado zinatimia kuni kupikia. Takriban familia 8 kati ya 10 hutegemea kuni kila siku, na ni familia 3 tu kati ya 10 zilizo na umeme.
- ⇒ Matumizi yetu ya kuni yanaharibu misitu. Kila msimu wa kiangazi, tunakata miti sawa na takriban ekari 6,500. Shule zetu nazo hutumia kuni nyingi kupika chakula, jambo linaloongeza tatizo.
- ⇒ Miti inapungua kwa kasi. Mwaka 2000, tulikuwa na miti mingi karibu 14%, lakini kufikia mwaka 2022 miti hiyo imepungua hadi 11%. Wakati huohuo, maeneo ya ardhi wazi na kavu yameongezeka kutoka 29% hadi 56%.
- ⇒ Upungufu wa miti unaathiri ardhi na wanyamapori. Tukikosa miti, mvua hupungua, mchanga huoshwa, na wanyamapori hukosa makazi ya kupita au kula.
- ⇒ Wanawake na wasichana wanapata mzigo mkubwa. Kila wiki hutumia zaidi ya saa 12 kutafuta kuni. Wanaweza kujeruhiwa na miiba au kukutana na wanyama hatari. Pia, uchovu kutoka na na kazi hii huathiri afya yao.

Sababu Za Kuhitaji Mabadiliko



- * Jamii yetu bado inategemea kuni na mkaa kwa matumizi ya kila siku.
- * Tukikosa kuchukua hatua sasa, ifikapo mwaka 2030, ardhi yetu itakuwa kame zaidi, ekari 32,000 za miti zinaweza kutoweka, sawa na kukata miti kati ya milioni 1.6 hadi 3.3.
- * Hili litaathiri mazingira yetu, wanyamapori, na maisha yetu ya kila siku.
- * Bei ya mafuta kama taa na dizeli inaweza kupanda zaidi na kufanya maisha kuwa magumu.
- * Zaidi ya hayo, moshi kutoka kwa kuni na mkaa unaathiri afya ya watu wetu. Moto wa kupikia unatumika ndani ya nyumba husababisha matatizo ya kupumua, hasa kwa kina mama na watoto wadogo walioko karibu na moto.



Sisi kama Jamii ya Kuku – Tunachoweza Kufanya Wenyewe



- ◇ **Tumia Nguvu Safi Majumbani:** Jaribu taa za sola, majiko bora au biogesi kama unaweza. Hata mabadiliko madogo kama kutengeneza briketi yanaweza kupunguza hitaji la kuni.
- ◇ **Shiriki Miradi ya Jamii:** Tushirikiane na mashirika kama MWCT au hifadhi za jamii. Tukihudhuria mafunzo kuhusu majiko bora, sola, au upandaji miti, tutapata ujuzi muhimu.
- ◇ **Heshimu Sheria za Uhifadhi:** Tukubaliane na kuzingatia sheria zetu, kama vile kukusanya kuni kavu tu, kutopiga mkaa kiholela, na kila kaya kupanda miti kila mwaka.
- ◇ **Wajengee Wanawake na Vijana Uwezo:** Wanawake wapewe nafasi ya kuongoza maamuzi ya kupika kwa njia safi. Vijana wasaidie kupanda miti, kueneza elimu, na kujifunza ujuzi mpya.

Tunachohitaji kutoka kwa Viongozi na Washirika:

- ◇ **Jumuisha Nguvu Safi kwenye Mipango ya Maendeleo:** Mipango ya Kaunti izingatie sola, LPG, na upandaji miti vijijini kama Kuku.
- ◇ **Toa Msaada na Motisha:** Tupe usaidizi wa vitendo kama ruzuku, mikopo au vikundi vya kusaidiana ili tuweze kutumia nishati mbadala.
- ◇ **Toa Mafunzo na Kazi za Vijana:** Fundisheni vijana wetu jinsi ya kufunga sola, kutengeneza biogesi au kujenga majiko bora, hii itasaidia kuunda ajira safi.
- ◇ **Tufungulie Fursa:** Hakikisha Kuku inanufaika na miradi ya wahisani, mipango ya serikali ya nishati safi, au misaada ya taasisi.
- ◇ **Tuwezeshe Kujifunza kwa Kuona:** Tupeni nafasi ya kutembelea jamii nyingine zilizofanikiwa kutumia nishati safi, kuona ni kuamini, na tunaweza kujifunza mengi.



Pamoja, Tunaweza Kuendeleza Jamii



Sisi watu wa Kuku tuna uwezo wa kujenga maisha bora. Tukishirikiana, tunaweza kucha kukata miti ovyo, kutumia nishati safi kama sola na biogesi, na kurejesha misitu yetu. Kila mmoja ana nafasi; mama anayepika kwa jiko safi, kijana anayepanda mti, au mzee anayeongoza jamii.

Hebu tufikirie Kuku mpya: nyumba zinazoangaza kwa taa za sola, watoto wakipumua hewa safi, vilima vyetu vikiwa na miti, na wanawake wakiongoza biashara za nishati safi. Hii inawezeka na tukishikamana; familia, wazee, vijana na viongozi.

Jamii yetu ni imara na ina busara. Sasa ni wakati wa kuchukua hatua. Tuseme: Nishati yetu italinda misitu yetu, na misitu yetu italinda maisha yetu ya baadaye. Tukifanya kazi pamoja, Kuku itakuwa mfano bora wa maisha safi na uhifadhi wa mazingira.

“Wakati bora wa kupanda mti ulikuwa miaka 20 iliyopita. Wakati wa pili bora ni sasa.” Tuchukue hatua leo kwa ajili ya kesho iliyo bora.

Kupanda Miti Upya: Wajibu wa Kila Mtu

Kupanda miti tena ni muhimu kwa kurejesha ardhi ya Kuku na kulinda mazingira yetu kwa vizazi vijavyo. Jamii inaweza kuongoza kwa njia zifuatazo:

- ◇ **Kulea Miche:** Kituo cha jamii kinaweza kukuza miche ya miti ya asili. Vikundi vya wanawake na vijana wanaweza kukusanya mbegu na kuilea kwa kutumia maarifa ya wazee. Hii inaweza kuwa chanzo cha kipato pia.
- ◇ **Kupanda kwa Wakati Sahihi:** Miti inapandwa vizuri mwanzoni mwa msimu wa mvua (Machi au Novemba), hasa kando ya mito, mashuleni, na karibu na nyumba. Maeneo ya pamoja yanaweza kuteuliwa kuwa misitu ya jamii au sehemu za miti ya kuni.
- ◇ **Kuhifadhi Miti:** Miti michanga hulindwa dhidi ya mifugo na ukame kwa kutumia uzio rahisi wa miiba au waya. Wanajamii wanaweza kumwagilia kwa kutumia maji ya matumizi ya nyumbani kama ya kuoshea vyombo. Miche iliyokufa ibadilishwe msimu ujao.
- ◇ **Kuhusisha Wote:** Kupanda miti ni jukumu la kila mtu. Vijana na watoto wahusishwe ili kuendeleza utamaduni wa uhifadhi. Shule zinaweza kuanzisha kluba za mazingira na kila mwanafunzi apewe jukumu la kupanda au kutunza mti.

Chaguzi Mbadala za Nishati Safi kwa Jamii ya Kuku:

Jamii ya Kuku imebarikiwa na jua kali, mifugo mingi, na watu wabunifu. Tunaweza kutumia rasilimali hizi kutatua changamoto ya nishati bila kuharibu misitu yetu.

◇ Nishati ya Jua (Solar):

Kuku hupata jua kali mwaka mzima. Tunaweza kutumia umeme wa jua kuwasha taa, kuchaji simu, kusikiza redio na hata kusukuma maji kutoka kwenye visima. Tayari familia nyingi Kuku zinatimia taa za sola au mifumo midogo ya sola nyumbani.

◇ Biogesi:

Kwa kuwa tuna ng'ombe, mbuzi na kondoo, tunaweza kutumia samadi kutengeneza gesi safi ya kupikia. Biogesi haina moshi na joto lake ni kali. Mabaki ya biogesi pia ni mbolea nzuri kwa bustani au malisho. Hii inaweza kusaidia kupunguza ukataji wa miti kwa kiasi kikubwa.

◇ Majiko Bora na Briketi:

Majiko bora yanapika kwa kutumia kuni au mkaa kidogo sana ikilinganishwa na jiko la mawe matatu. Pia yanatoa moshi kidogo, hivyo ni salama kwa afya na mazingira. Kwa kutumia briketi au majiko haya, tunaweza kupunguza matumizi ya kuni kwa asilimia 30 hadi 50.

Faida za Kupika kwa Njia Safi

Kubadili kutoka kwa kuni na mkaa kwenda kwa njia safi za kupikia siyo tu kunalinda miti, kunaboresha afya yetu, maisha yetu, na mazingira yetu.



Tunapunguza Ukataji wa Miti


Jiko bora au nishati mbadala kama briquettes, biogas au jiko la jua hutumia kuni kidogo sana. Kama familia nyingi zitapika kwa njia hizi, tutakata miti chache zaidi. Misitu yetu itapona, ardhi kavu itaanza kuota tena, na tutarudisha kijani cha Kuku.

Tunaboresha Afya Yetu

Kupika kwa moto wa wazi hutoa moshi mwingi ndani ya nyumba. Hii husababisha kikohozi, mafua ya mara kwa mara, na kuwashwa kwa macho. Jiko safi kama biogas, LPG, au jiko lenye bomba la moshi hutoa moshi kidogo au hakuna kabisa, hivyo familia zinapumua hewa safi na kubaki na afya bora.

Tunapunguza Muda na Uchovu

Wanawake na wasichana hutumia saa nyingi kila wiki kutafuta kuni. Kwa kutumia nishati safi, muda huo huokolewa. Wanaweza kutumia muda huo kwa masomo, kazi, familia au kupumzika..



KUKU GROUP RANCH

Imeandaliwa na: S. Vintage W. Mwangi-
LDE Thesis Lab, Chuo Kikuu cha Nairobi
Kwa msaada kutoka Kituo cha Uvumbuzi
cha Nuvoni, MWCT na Jamii ya Kuku
Group Ranch.

Email: vintagemwangi5@gmail.com

Nishati Yetu, Misitu Yetu, Mustakabali Wetu

Chaguo Tunalofanya Leo:

- 1) jinsi tunavyopika,
 - 2) nishati tunayochagua kutumia,
 - 3) na jinsi tunavyotunza ardhi yetu,
- vitaathiri mustakabali wa familia zetu, misitu yetu, na riziki zetu.

Tuchague nishati safi, tulinde mazingira yetu, na tushirikiane kwa ajili ya Kuku iliyo na afya, yenye kijani kibichi, na ustawi mkubwa. .

Mustakabali uko mikononi
mwetu.



Chaguo za Nishati Safi kwa Kuku



Nguvu ya
Jua



Nishati ya
Biogesi



Makaa Mbadala
na Jiko Bora

NISHATI SAFI NA UHIFADHI WA MAZINGIRA KATIKA RANCHI YA KUKU

Kuwasha nyumba zetu, kulinda miti yetu,
na mustakabali wetu.



KUKU GROUP RANCH

Muhtasari wa Jamii: Nguvu Safi na Uhifadhi katika Ranchi ya Kuku

Muhtasari wa Jamii: Nguvu Safi na Uhifadhi katika Ranchi ya Kuku

Tuangaze boma zetu,
tulinde mazingira yetu,
tuimarisha nyumba zetu

